# Shindano la Video la Mo Money Mo Problems Climate Justice

*Heshima kwa Miaka 50ya Hip-Hop*

Mo' Money Mo' Problems: Climate Justice Remix Iliyoimbwa na Notorious B.F.C. (Black Femme Crew) Wakiadhimisha miaka 50ya Hip-Hop Wanafanya Wito wa Dharura wa Haki ya Tabia ya Nchi

Mo' Money Mo' Problems: The Climate Justice Remix ni mwigo wa, na shukrani kwa muziki wa, hip-hop wa Mo' Money Mo' Problems ulioimbwa na Notorious B.I.G., P. Diddy, na Ma$e, ambao kwa kiasi kikubwa umeiga Diana Ross' "I'm Coming Out," wimbo mwingine wa ajabu unaoongozwa na mwanamke!

Video yetu iko katika sehemu tatu. Aya ya kwanza ni mtazamo wa mpendwa Mama wa Dunia, akiweka mafuta ya kisukuku kwenye mlipuko na akisherehekea uwezo wa watu. Ya pili ni kutoka kwa mtazamo wa jamii na uwezo wa demokrasia. Aya ya tatu inahitimishwa kwa Mama Dunia na Jamii wakiungana pamoja kufanya kile kinachohitajika ili kupigania haki ya tabia ya nchi!

**CHANGAMOTO. SASA TUNAKUKARIBISHA ULETE MSANII (WASANII) UMPENDAYE ZAIDI WA HIP-HOP**

Tunalitanguliza Shindano la Video la Haki ya Hali ya Hewa la Mo Money Mo Problems

Hii hapa ni nafasi yako ya:

- Kutupa Chini Kipasa Sauti: Kutunga wimbo wako mwenyewe wa haki ya tabia ya nchi unaojumuisha Hip-Hop.
- Kunyoosha Misuli Yako ya Ubunifu: Kuunda video ambayo inaelimisha na kugusa mioyo.
- Kusimama na kufanya jambo: Kueneza ujumbe kuhusu haki ya hali ya hewa, kutetea mabadiliko na kuhamasisha jamii ya kimataifa.

**TCLP:** ***Shindano la Video la Mo' Money, Mo' Problems Climate Justice*** linakualika ujitokeze na kunyoosha misuli yako ya ubunifu ili kuwasilisha ujumbe wa kuvutia kuhusu haki ya tabia ya nchi kupitia wimbo na video ya mtindo wa Hip-Hop!

## Zawadi na Tarehe Kuu:

- Nafasi ya kwanza (1): $10,000
- Nafasi ya pili (1): $5,000
- Nafasi ya tatu (1): $2,000
- Wahindani 3: $1,000 kila mmoja wao

- Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha: November 24
- Kipindi cha Kupiga kura: Novemba 27 hadi 30 (Upigaji kura wa umma + paneli tukufu ya waamuzi)
- Tangazo la Mshindi: Desemba 4, (ikiambatana na uchunguzi wa mtandaoni na wa moja kwa moja kwenye UNFCCC COP 28)

Video zilizoshinda zitatangazwa mnamo Desemba 4, 2023, mtandaoni na kwenye Kongamano la 2023 la Umoja wa Mataifa la Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC COP 28), kwa uchunguzi wa video zote kwenye UNFCCC COP 28 na Tangazo la Ulimwengu mzima la mtandaoni!

Lazima wagombeaji na washiriki wote wawe na umri wa miaka 18 au zaidi ili kuingia.

## Jinsi ya Kuingia

**Changamoto:**
Unda video ya kiwango cha chini cha dakika 2 (sekunde 120) na isiyozidi dakika 5 na sekunde kumi na tano (sekunde 315)ukijibu shindano hili.

Mawasilisho ya kikundi lazima yawe na kiongozi wa timu aliyeteuliwa kwa ajili ya mawasiliano kuhusu masuala ya kiufundi na kiusimamizi na inapohitajika kwa arifa ya mshindani wa fainali na mshindi.

Hakuna vizuizi kuhusu jinsi utakavyoiunda video yako. Unaweza kuzungumza kwenye kamera, kutumia vifaa, kujumuisha uhuishaji, n.k Lengo ni kuwa mbunifu na kuwasilisha ujumbe unaovutia kuhusu haki ya hali ya hewa kupitia wimbo na video ya mtindo wa Hip-Hop!

**Maelezo ya Video:**

1. Faili ya video inapaswa kuwa: Mada ya Wimbo_Jina la Mwisho_Jina la Mwanzo la mtu binafsi anayewasilisha au kiongozi wa timu, kama inavyofaa.
2. Video zinazowasilishwa hazipaswi kuwa fupi kuliko dakika 2 (sekunde 120) na hazipaswi kuzidi dakika 5 na sekunde kumi na tano (sekunde 315) kwa urefu. Video zilizo nje ya kiwango hiki hazitastahiki kuzingatiwa.
3. Lazima wagombeaji na washiriki wote wawe na umri wa miaka 18 au zaidi ili kuingia.
4. Video zinapaswa kuchukuliwa na kuhaririwa katika umbizo la mwonekano wa ubora wa juu (HD 1290x720 au zaidi).
5. Changamoto inafunguliwa mnamo Oktoba 31, 2023.
6. Wasilisha video yako kwa kubofya hapa kufikia Novemba 18, 2023.

**Waamuzi:**

Washiriki watatathminiwa kulingana na uwasilishaji ujumbe na mawasiliano yao, ubunifu na ubora wa video na uhariri. ***Mo' Money Mo' Problems: The Climate Justice Remix*** ni mfano wa aina ya ujumbe tunaoutafuta!

Waamuzi wa shindano hili watajumuisha viongozi wa haki ya tabia ya nchi na mazingira. Umma pia utaruhusiwa kupiga kura! Uamuzi utafanyika kutoka Novemba 21, 2023 – Novemba 26, 2023.

## Sheria na Miongozo

Washiriki na wagombeaji wote wanahitajika kupitia sheria na miongozo hii kabla ya kuingia katika shindano hili. Uwasilishaji wako utachukuliwa kuwa kukiri na kukubali kwako kwa sheria na miongozo hii. Mwasilisho ambayo hayazingatii sheria na miongozo ifuatayo yataondolewa. Mradi wa Chisholm Legacy hauko chini ya wajibu wowote wa kujibu madai au maswali yoyote kuhusu matokeo ya shindano. Mradi wa Chisholm Legacy una usemi wa mwisho kuhusu hoja yoyote isiyoonyeshwa katika sheria ya kuingia.

- Video zinazoingia hazipaswi kuwa fupi kuliko dakika 2 (sekunde 120) na hazipaswi kuzidi dakika 5 na sekunde kumi na tano (sekunde 315) kwa urefu.
- Mradi wa Uridhi wa Chisholm una haki, kwa uamuzi wake pekee, ya kumuondoa mtu yeyote binafsi watakayetambua kuwa anatatiza mchakato wa kuingia, shughuli ya shindano, taratibu za upigaji kura, paneli ya waamuzi, au tovuti ya Mradi Chisholm Legacy.
- Wasilisho moja kwa kila mtu binafsi/timu. Ikiwa utawasilisha kama mtu binafsi, huwezi pia kuwasilisha kama mmoja wa timu nyingine na kinyume chake.
- Lazima wagombeaji na washiriki wote wawe na umri wa miaka 18 au zaidi.
- Lazima mawasilisho yawe kazi halisi ya timu au mtu binafsi, kamwe hayapaswi kukiuka haki za wahusika wengine, lazima ziwe zinafaa kuonyeshwa kwa umma na zisiwe chafu. Mawasilisho hayapaswi kuwa na kauli za kashfa kuhusu mtu, shirika, au kitu na hayapaswi kuingilia haki za faragha au haki zingine za mtu, shirika au kitu chochote. Mawasilisho yaliyo na maudhui yaliyopigwa marupuku au yasiyofaa kama ilivyoamuliwa na paneli ya waamuzi, kwa uamuzi wao wenyewe, hayatastahiki na yataondolewa na Mradi waChisholm Legacy.
- Ni kura moja tu kwa kila mtu inayoruhusiwa kwa upigaji kura wa umma. Upigaji kura wa umma wa video za fainali utafunguliwa kuanzia Novemba 21, 2023 – Novemba 26, 2023.
- Licha ya hayo yaliyotangulia, watu wafuatao HAWASTAHIKI kuingia katika mashindano ya Mradi wa Urithi wa Chisholm, hata kama watu hao wanatimiza mahitaji yaliyopeanwa hapo juu.
  a) Wafanyakazi wowote (yaani, wa muda kamili, wa muda na/au wafanyakazi wa muda mfupi), wanakandarasi wa kujitegemea, au wanachama wa bodi ya, Mradi wa Uridhi wa Chisholm; b) Mwanafamilia yeyote wa karibu wa wafanyakazi hao,wanakandarasi wa kujitegemea, au wanachama wa bodi, ikijumuisha bila kikomo wanandoa wa sasa na/au waliotengana, wazazi, babu na nyanya, watoto, wajukuu, ndugu na dada, wakwe, na/au jamaa kwa njia ya ndoa katika yoyote ya aina zilizotangulia; na c) Mtu yeyote binafsi anayeishi kihalali katika kaya sawa (yaani, kwenye anwani sawa) ya wafanyakazi hao, wanakandarasi wa kujitegemea, au wanachama wa bodi, ikijumuisha bila kikomo wanaokaa kwa chumba kimoja, wanaokaa kwa nyumba moja, watu wengine muhimu na washirikal.

## Sheria na Masharti ya Kawaida

Washiriki na wagombeaji wote wana haki ya nyimbo na/au video zao, lakini kwa kuwasilisha wimbo au video, wasilisho hili linaupa Mradi wa Chilsom Legacy leseni isiyo ya kipekee, isiyoweza kubatilishwa ya kunakili, kutoa, kuonyesha, au kusambaza wasilisho na kufanya kazi zingine zinazohusiana kwa wasilisho au sehemu kuu ya wasilisho bila ruhusa ya mapema. Mradi wa Chisholm Legacy utamhusisha mgombeaji na kazi yoyote inayohusika.

Ikiwa idadi isiyotosha ya mawasilisho itapokelewa, Mradi wa Chisholm Legacy una haki ya kurekebisha au kughairi shindano kabla ya kutangaza washindi.

Uamuzi wa waamuzi utachukuliwa kuwa wa mwisho na hakuna kukata rufaa au mapitio mapya yatakayoruhusiwa.

Wagombeaji wote wanakubali kuwa, warithi wao na mali yao, hawatawadhuru wafanyakazi wa Mradi wa Chisholm Legacy kwa majeraha yoyote na yote na/au malalamiko yanayotokana na kushiriki katika shindano hili. Kwa kuwasilisha wasilisho, wawasilishaji wote wanaidhinisha kuwa wamepokea ridhaa kutoka kwa kila mtu atakayejitokeza, ambaye anaonekana, au sauti yake inasikika katika video zao zilizowasilishwa.

Washindi wataarifiwa kupitia barua pepe au simu mnamo au karibu Novemba 30, 2023 na watahitajika kujaza toleo la utangazaji na hati zingine kama hizo kama inavyoweza kuhitajika na Mradi wa Urithi wa Chisholm ili kulinda haki yake ya kutangaza na kutumia wasilisho litakaloshinda. Hati zinazohitajika lazima zitiwe sahihi na kupokewa ndani ya siku saba (7) za kalenda za siku iliyochapishwa kwenye arifa ya mshindi. Kukosa kutii huenda kukasababisha kunyang'anywa kwa utambuzi na usambazaji wa kitaifa na uchaguzi wa wasilisho linalofuata la juu zaidi kama ilivyo lengo. Ikiwa mshindi hawezi kufikiwa ndani ya siku tano (5) za kalenda za jaribio la kwanza la arifa, ikiwa arifa itarejeshwa kama isiyowasilishwa, ikiwa mshindi atakataa arifa au ikiwa hatazitii sheria na miongozo hii ya shindano, atanyang'anywa hali ya ushindi na uchaguzi wa mshiriki mwingine aliye na alama ya juu uatafanyika.

Usijumuishe video au muziki mwingine katika video zako bila ruhusa. Kwa kuwasilisha wasilisho, kila wasilisho linaidhinisha kuwa yeye ni mwandishi wa pekee na mmiliki wa hakimiliki ya wasilisho au ana ruhusa (kupitia leseni au vinginevyo) ya kutumia au kujumuisha sehemu hizo za wasilisho zilizoandikwa au kumilikiwa na wahusika wengine. Ingawa matumizi ya picha, muziki na kazi zingine zilizo katika umma huenda yakajumuishwa katika mawasilisho, nyenzo zinazokiuka haki za mhusika mwingine yeyote huenda zisitumike.

Washindi wana wajibu wa ushuru wote au ada zingine zinazohusiana na zawadi wanayopokea.

Sera ta Faragha: Mradi wa Urithi wa Chisholm hautashiriki maelezo yako ya mawasiliano na wahusika wengine bila ruhusa yako.

## Sehemu za Fomu ya Wasilisho

Wasilisha video yako kwa [kubofya hapa]

Weka idadi jumla ya nambari ya watu wanaoshiriki katika wasilisho lako. Tafadhali weka nambari kutoka 1 hadi 25

Orodhesha majina yao halali, moja kwa kila mstari

Jina la Msanii au kikundi

Barua pepe ya Msingi ya Mawasiliano (Inahitajika)

Nambari ya Msingi ya Simu ya Mawasiliano

Toa kiungo cha video yako (inahitajika) Shiriki kiungo kwenye Dropbox, YouTube, Vimeo, au tovuti zingine ambapo mtu anaweza kuifikia na kuipakua.

Mada ya Wimbo (Inahitajika)

Ridhaa (Inahitajika)

Msanii/kikundi kinachowasilisha kinakubaliana na sheria na masharti ya shindano (tazama Sheria na Miongozo hapo juu)

Bofya Wasilisha utakapokuwa tayari